

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

FURSA YA KUOMBA NAFASI YA UJUMBE KATIKA BARAZA WAKILISHI LA VIJANA LA SHIRIKA LA KIMATAIFA LA MAWASILIANO (ITU GENERATION CONNECT ENVOY)

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama mwanachama wa ITU, TCRA imepokea fursa kutoka ITU ya kupendekeza watanzania watakaokidhi vigezo vya nafasi ya ujumbe katika Baraza wakilishi la Vijana la ITU (ITU Generation Connect Envoy). Waombaji wa nafasi hiyo wanapaswa kuwa watanzania wenyewe umri kati ya miaka 18 na 24 ambao wanashauku ya kuwa sehemu ya Baraza tajwa.

Waombaji wanatakiwa kueleza na kutoa ushahidi wa kujitolea na kushiriki kwao katika kutumia TEHAMA kwa malengo ya kielimu, maendeleo ya kijamii na uchumi, au uwezeseshaji wa vijana. Kujitolea huko kunaweza kudhihirishwa kwa njia nyingi, kama vile kupata na kusambaza maarifa, kushiriki katika shughuli za kijamii zinazohusisha TEHAMA, au kubuni, kutengeneza, na kuendesha programu maalum (pamoja na zile zinazoendelea) au miradi yenye kuleta tija kijamii, kitaifa, kikanda, au kimataifa.

Kwa waombaji wanaopenda kuchukua fursa hii, tafadhali wawasilishe maombi yao kwa TCRA kuitia anwani ya barua pepe ya generationconnect@tcra.go.tz kabla au ifikapo Jumapili, Februari 4, 2024. Aidha, kulingana na vigezo tajwa, waombaji wanne (4) watachaguliwa na TCRA na kupendekezwa ITU ili washiriki kuomba nafasi ya ujumbe moja kwa moja katika Baraza wakilishi la Vijana la Shirika la Kimataifa la Mawasiliano kabla ya Jumamosi, Februari 10, 2024.

TCRA inawahimiza wadau wote, ikiwa ni pamoja na wanachama wa vilabu vya kidijiti, Sekta binafsi, Vyuo vikuu, vituo vya uvumbuzi, na taasisi za Umma, kuhimiza watu wanaokidhi sifa hizi kuomba nafasi hii.

Maelezo zaidi kuhusu fursa hii yanapatikana katika tovuti <https://www.itu.int/md/D22-BDT-CIR-0018/en>. Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kuitia namba 0800008272 au barua pepe dawatilahuduma@tcra.go.tz.

Ukomo wa mawasilisho yote ni Jumapili, Februari 4, 2024

Imetolewa tarehe **29 Januari 2024**.

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU